**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

## HATUA ILIYOFIKIWA KATIKA MAANDALIZI YA DIRA YA TAIFA YA MAENDELEO 2050 NA HATUA ZINAZOFUATA

***Ijumaa, 06 Disemba 2024***

1. Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo inaendelea kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2000-2025, ambayo imekuwa ikiongoza mipango ya maendeleo ya nchi katika kipindi cha miaka 25 iliyopita. Utekelezaji wa Dira hii utafikia tamati ifikapo mwisho wa mwaka 2025.

2. Kufuatia kuelekea kukamilika kwa utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2000-2025, kwa kuzingatia Sheria ya Tume ya Mipango (Kifungu cha 6[2b]), Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alielekeza Serikali kuanza mchakato wa kuandika Dira nyingine itakayoongoza mipango ya maendeleo ya Taifa kwa miaka mingine 25 (au zaidi) ijayo.

3. Mchakato wa kuandika Dira ya Taifa ya Maendeleo kuelekea mwaka 2050 unazingatia hatua kumi na moja zifuatazo:-
   - *(i)* ***Kuandaa na kuidhinishwa kwa miongozo ya kuandika Dira***
   - *(ii)* ***Kuzinduliwa rasmi wa mchakato wa kuandika Dira ya Taifa ya Maendeleo kuelekea mwaka 2050*** tarehe 03 Aprili 2023 uliofanywa na Mheshimiwa Dkt. Philip Isidor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(iii) ***Kuunda vyombo vya kitaasisi vya kuandika Dira.*** Mchakato wa Dira unasimamiwa katika ngazi tatu, ambazo ni Sekretariati iliyo chini ya Tume ya Taifa ya Mipango, Timu Kuu ya Wataalam, na Kamati ya Uongozi ya Dira iliyo chini ya uenyekiti wa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

(iv) ***Kufanya tathmini ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2000-2025***. Taarifa ya tathmini hii ilizinduliwa rasmi tarehe 09 Disemba 2023 na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, katika siku hii Mheshimiwa Rais alizindua rasmi nyenzo za kukusanya maoni ya wadau.

(v) ***Kukusanya maoni ya wananchi na wadau wa maendeleo***. Hadi kufikia mwezi Oktoba 2024 jumla ya wananchi na wadau 1,170,970 walitoa maoni yao kwa njia zifuatazo:

a) Tafiti katika ngazi ya kaya: *15,483*
b) Ujumbe kwa njia ya simu (USSD) *1,118,978*
c) Tovuti 13,459
d) Makongamano 12 yaliyohudhuriwa na watu 22,779
e) Mahojiano mahsusi na ya kina na viongozi mbalimbali waliopo madarakani na waliostaafu: 44
f) Mikutano na semina: 220
g) Nyaraka zilizokusanywa: 33.

(vi) ***Kujifunza kutoka nchi mbalimbali zilizopiga hatua kubwa kimaendeleo*** kutoka mabara ya Afrika, Asia, Ulaya na Amerika

(vii) ***Uchambuzi, uandishi na uhariri a taarifa mbalimbali***

(viii) ***Rasimu ya Dira 2050 kuzinduliwa na kukusanya maoni ya ziada katika ngazi ya uhakiki (validation)***

(ix) ***Taarifa na Rasimu ya Dira kujadiliwa na kufanyiwa maamuzi na vyombo vya vya maamuzi vya Serikali***

(x) ***Taarifa na Rasimu ya Dira kuwasilishwa, kujadiliwa na kuidhinishwa na Bunge***.

(xi) ***Kuzinduliwa rasmi kwa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050***

4. Maoni ya wananchi na wadau yalitolewa katika maeneo makubwa manne yafuatayo:-

   *(i)* Tathmini ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 kwa kuzingatia maeneo tuliyofanikiwa na changamoto zilizojitokeza

   *(ii)* Hali ya nchi ya sasa

   *(iii)* Matarajio na matamanio kuelekea 2050

   *(iv)* Vipaumbele vya kuzingatiwa.

5. Matamanio na matarajio ya wananchi na wadau ni katika maeneo makubwa matano yafuatayo:

   *(i)* Uchumi imara, unaostawi na unaoboresha maisha yao

   *(ii)* Huduma bora za jamii (elimu na afya)

   *(iii)* Utawala bora, utoaji haki, ulinzi na usalama

   *(iv)* Maendeleo ya teknolojia na ubunifu

   *(v)* Ulinzi na matumizi endelevu ya raslimali za taifa.

6. Wananchi na wadau walitaja sekta tano zifuatazo za kuzingatiwa kama vipaumbele vya kitaifa kuelekea mwaka 2050:

   *(i)* Kilimo

   *(ii)* Uzalishaji viwandani (kuongeza thamani)

   *(iii)* Miundombinu

   *(iv)* Huduma bora za jamii

   *(v)* Madini, mafuta na gesi

7. Kwa kuzingatia maoni ya wananchi na wadau mbalimbali, taarifa za kitafiti na uzoefu kutoka nchi mbalimbali zilizopiga hatua kubwa za kimaendeleo, Kamati Kuu ya Kitaalam imeandaa Rasimu ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

8. Rasimu ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 (Dira 2050) itazinduliwa rasmi tarehe 11 Disemba 2024 katika Hoteli ya Golden Tulip, Zanzibar. Mgeni Rasmi katika tukio hili atakuwa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

9. Aidha, uzinduzi wa Rasimu ya Dira 2050 utaenda sambamba na uzinduzi wa awamu ya pili ya kukusanya maoni ya wadau. Awamu hii itahusu maoni ya uhakiki wa Rasimu ya Dira 2050 (validation).

10. Zoezi la kukusanya maoni ya uhakiki litahitimishwa tarehe 18 Januari 2025 kwa Waziri Mkuu kupokea rasimu ya pili ya Dira 2050 iliyoboreshwa kutonana na maoni ya wadau katika hatua ya uhakiki.

11. Januari - Machi 2025 Rasimu ya Dira 2050 itajadiliwa na kufanyiwa maamuzi katika vyombo vya serikali (Makatibu Wakuu, Tume ya Taifa ya Mipango na Baraza la Mawaziri).

12. Aprili-Mei 2025 Rasimu ya Dira 2050 itapokelewa, kujadiliwa na kuidhinishiwa rasmi na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

13. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anatarajiwa kuzinduwa rasmi Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 mwezi Mei/Juni 2025.

14. Maandalizi ya Dira 2050 yanaenda sambamba na maandalizi ya ***Mpango Elekezi wa Muda Mrefu wa Maendeleo*** (***Long-Term Perspective Plan – LTPP***) utakaotafsiri maono na matamanio yaliyopo katika Dira 2050.

***Dira hii ni ya Watanzania wote na naomba kuwasihi Watanzania wote washiriki kikamilifu katika hatua zote hadi siku rasmi ya Uzinduzi*.**

***Imetolewa na:***

Prof. Kitila Alexander Mkumbo **(Mb.),**

**WAZIRI WA NCHI,**
**OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI.**

**Dar Es Salaam, ijumaa 06 Disemba 2024**

*Kwa mawasiliano na taarifa zaidi:*

**Thobias Makoba,**
**Msemaji Mkuu wa Serikali,**
**Simu: +255 (0)** 758 800 883
**Email:** thobias.makoba@mawasiliano.go.tz